East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1345

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mitindo ya Lugha Inayowabainisha Wahusika Wazimu katika Riwaya za Habwe

*Joseph Ondiek Odhong'*[1*], *Debora Nanyama Amukowa*[1] *na Beverlyne Asiko Ambuyo*[1]

[1] Chuo Kikuu cha Maseno, S. L. P. 333, Maseno, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: josephondiekodhong@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1345**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*31 Juli 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Motifu, Wahusika wazimu, Mitindo, Uumbaji.*

**IKISIRI**

Takwimu za Shirika la Afya Ulimwenguni zinaonyesha ongezeko la idadi ya wazimu katika jamii duniani kote (Kovacevic, 2021). Waandishi wa fasihi wamewaumba wahusika wazimu wakiakisi mazingira wanamoishi. Tangu jadi wahakiki wamejitahidi kueleza vipi wahusika wazimu wametumika katika fasihi. Tahakiki za tamthilia za Shakespeare na za Kiingereza za karne ya ishirini zimeeleza namna na sababu za uumbaji wao. Katika riwaya za Kiswahili hakuna tahakiki zinazoshughulikia wahusika wazimu wala mitindo ya lugha inayowabainisha. Makala hii ilidhamiria kuchanganua mitindo ya lugha inayowabainisha wahusika wazimu katika kazi teule za Habwe. Uteuzi huu ulitokana na Habwe kusifiwa kuwa mwandishi wa fasihi ya kiongofu aliyetumia motifu ya wazimu katika riwaya zake (Gromov, 2018). Riwaya tano za Habwe: Paradiso (2005), Cheche za Moto (2008), Fumbo La Maisha (2009), Safari ya Lamu (2011) na Kovu Moyoni (2014) ziliteuliwa kupitia usampulishaji dhamirifu kwa kuwa zilikuwa na wahusika wazimu. Nadharia ya umitindo iliyoasisiwa na Bally (1909) ) na kuendelezwa na Thornborrow na Wareing (1998) iliteuliwa kwa ajili ya kazi hii. Muundo wa kiuchanganuzi umetumiwa. Data zilikusanywa kutumia kifaa cha kudondoa data kilichokuwa na vidokezo vya mitindo ya lugha inayotambulisha wahusika wazimu. Matini ya riwaya teule imesomwa kwa makini na vipengele mbalimbali, kurekodiwa. Kisha data imechanganuliwa, kufasiriwa na kuratibiwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Matokeo yamewasillishwa kwa njia ya maelezo. Makala hii imedhihirisha jinsi mitindo ya lugha ilivyotumiwa kuwatambulisha wahusika wazimu.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1345

**APA CITATION**

Odhong', J. O., Amukowa, D. N. & Ambuyo, B. A. (2023). Mitindo ya Lugha Inayowabainisha Wahusika Wazimu katika Riwaya za Habwe *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 243-258. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1345.

**CHICAGO CITATION**

Odhong', Joseph Ondiek, Debora Nyanyama Amukowa and Beverlyne Asiko Ambuyo. 2023. "Mitindo ya Lugha Inayowabainisha Wahusika Wazimu katika Riwaya za Habwe". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 243-258. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1345.

**HARVARD CITATION**

Odhong', J. O., Amukowa, D. N. & Ambuyo, B. A. (2023) "Mitindo ya Lugha Inayowabainisha Wahusika Wazimu katika Riwaya za Habwe", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 243-258. doi: 10.37284/jammk.6.1.1345.

**IEEE CITATION**

J. O., Odhong', D. N., Amukowa & B. A. Ambuyo, "Mitindo ya Lugha Inayowabainisha Wahusika Wazimu katika Riwaya za Habwe", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 243-258, Jul. 2023.

**MLA CITATION**

Odhong', Joseph Ondiek, Debora Nyanyama Amukowa & Beverlyne Asiko Ambuyo. "Mitindo ya Lugha Inayowabainisha Wahusika Wazimu katika Riwaya za Habwe". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Jul. 2023, pp. 243-258, doi:10.37284/jammk.6.1.1345.

## UTANGULIZI

Wahakiki wengi wameandikia wahusika wa kifasihi wakieleza maana, dhima na aina. Kwa mfano Wamitila (2002) ameeleza wahusika kuwa viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi, na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda. Rono (2013) anaeleza kwamba wahusika wanasawiriwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Watuha (2022) ameeleza aina za wahusika katika fasihi: wahusika wakuu, wahusika wasaidizi, wahusika vinyago, wahusika bapa na wahusika duara. Kati ya tafiti zilizoko za fasihi ya Kiswahili hakuna kazi inayohusu wahusika wazimu wala hakuna tahakiki yoyote iliyofanywa kuhusu lugha inayowabaini wahusika wazimu. Utafiti huu umedhamiria kujaza pengo hilo

Mtu kuwa mwendawazimu ni hali ambapo mwathiriwa ametengwa na uhalisia asiweze kuelewa maana sawa na watu wengine wala kuathirika nayo (Milner, 1987). Gelder et al. (2001) anaeleza aina kadhaa za wazimu kama vile: wazimu wa kimwenendo kutokana na matumizi ya madawa ya kulevya na wazimu wenye kuathiri mfumo wa neva unaotokana na mfadhaiko. Wahusika wazimu katika kazi hii utakuwa na maana ya wale walioumbwa na kupewa lugha na matendo kama ya wazimu na kutumiwa kuwasilisha maudhui ya kifasihi.

Wahusika wendawazimu wametumiwa na waandishi tangu jadi, kila wakati wakisawiriwa tofauti tofauti na kupewa nafasi anuwai (Kramer, 2014)). Namna wanavyoumbwa na kutumiwa, asemavyo Feder (1980), hutegemea dhamira ya msanii katika kazi yenyewe. Kwa mfano, Shakespeare aliumba wahusika wazimu katika tamthilia zake kama vile mwana mfalme na Hamlet na kutumia motifu hii kufumba ujumbe wake (Kramer, 2014). Uwezo wake wa kuwaumba ulitokana na welewa wake wa maendeleo ya kimatibabu (Morris, 2012).

Baada ya enzi hizo za kina Shakespeare, waandishi wameendelea kutumia wahusika wazimu katika kazi zao kwa sababu mbali mbali. Waandishi wa fasihi wa enzi za Malkia Viktoria wa Uingereza (1837 – 1901) walikuwa na hamu ya kuchangia uchunguzi wa hali ya wazimu wa mfalme George wa Tatu aliyeugua ugonjwa wa kiakili mnamo mwaka wa 1798 kwa sababu kufanya hivyo kuliwapa umaarufu katika kiwango cha kimataifa (Filson, 2014).

Kuna waandishi ambao hutumia wahusika wazimu ili kujieleza kuhusu hali wanazopitia kwa njia ya ubunifu. Sylvia Plath (1963, *The Bell Jar),* Jean Rhys (1966, *Wide Sargasso Sea*) na Janet Frame (1961, *Faces In The water*) ni kati ya waandishi ambao

waliaminika kuwa na matatizo ya kiakili wakabuni kazi za kifasihi ili kujieleza.

Uteuzi wa mada hii ulitokana na hamu ya kufafanua Matumizi ya lugha inayowabainisha wahusika wazimu. Kwa mujibu wa Gromov (2018), Habwe ni mwandishi wa fasihi ya kiongofu aliyetumia motifu ya wazimu katika riwaya zake. Jinsi ilivyokuwa kwa waandishi wenzake wanaowaumba wahusika wazimu, naye alikuwa na sababu zake kuwaumba. Ametumia mitindo ya lugha kuwabainisha wahusika wazimu katika riwaya zake tano zilizoteuliwa katika kazi hii.

Mitindo ya lugha kwa mujibu wa Lemon and Reis (1965) huhusisha kuangalia uteuzi wa msamiati na tamathali za semi. Tamathali za usemi ni usemi unaobadilisha maana dhahiri au za kawai da za maneno ili kuleta maana maalumu ya fasihi iliyokusudiwa na msanii (Madumulla, 2009). Makala hii ilidhamiria kuonyesha matumizi ya, istiari, tabaini, misemo, ritifaa, uzungumzi nafsia, tashbihi, taswira, mbinu rejeshi na maswali balagha kuwabainisha wahusika wazimu.

## UHAKIKI WA KINADHARIA

### Nadharia ya Umitindo

Nadharia ya umitindo iliyoasisiwa na Bally (1909) na kuendelezwa na Thornborrow na Wareing (1998) imetumiwa kama dira ya kuongoza kazi hii. Nadharia ya Umitindo hurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani kwa lengo mahususi. Kutokana na maoni ya wanaisimu na wahakiki walioshikilia kuwa taaluma hizi mbili; uhakiki wa kifasihi na kazi za kiisimu hazina uhusiano wowote, Leech alipata motisha wa kuandika kitabu chake, *A Linguistic Guide to English Poetry* (1969) ambamo alishughulikia suala la mtindo katika kuchanganua matini za kifasihi. Leech (1969) anasema kuwa umitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma, unaofungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu.

Wamitila (2008) ametoa mfano wa tamathali za usemi zinazohusisha ukiukaji wa aina fulani ambapo neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi. Anasisitiza mambo kadhaa kuwa muhimu zaidi katika uhakiki wa mtindo katika fasihi: lugha ya kitamathali, uteuzi wa mtindo, usimulizi na mtazamo. Mitindo ndiyo hutumiwa kuwasilisha dhamira na maudhui. Umitindo basi ni namna ya kuchanganua mtindo kisayansi hasa katika kazi za kifasihi. Kemunto (2016) anaeleza kuwa nadharia hii ya umitindo huonyesha umuhimu wa lugha katika kuelezea maana ya fasihi. Nadharia ya umitindo imekuwa faafu kuchanganua mbinu zilizotumiwa kuwabainisha wahusika wendawazimu katika kazi hii.

## MBINU ZA UTAFITI

Muundo uliozingatiwa katika utafiti huu wa kithamano ni muundo-elezi. Eneo kithematiki limekuwa wahusika wazimu katika utanzu wa riwaya. Kundi tafitiwa ni riwaya zote zilizoandikwa na msanii John Habwe. Usampulishaji dhamirifu unaozingatia sifa mahsusi za vitafitiwa kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) ulitumika na riwaya zenye matini kuhusu wahusika wazimu kuteuliwa. Nazo ni: *Paradiso*, *Cheche za Moto*, *Fumbo la Maisha*, *Safari ya Lamu* na *Kovu Moyoni*. Utafiti Maktabani ulivyopedekezwa na Bollo (2020) unaohusisha mambo ambayo tayari yameandikwa vitabuni, ulitekelezwa kwa kutumia kifaa cha kudondoa data kilichokuwa na vipengele vya mbinu za lugha. Kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti, data zimekusanywa, kuainishwa, kupangwa, kunukuliwa, kufasiriwa na kujadiliwa zikiongozwa na nadharia ya umitindo kama dira. . Kupitia uchanganuzi matini maelezo yametolewa kulingana na vipengee vilivyopatikana kwenye matini Uchanganuzi ulifanywa na data kuwasilishwa kuzingatia muundo – elezi.

## MATOKEO NA MAJADILIANO

### Mitindo ya lugha inayotumiwa Kuwabainisha Wahusika wazimu

Umitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma. Mitindo

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

inatawaliwa na lengo au nia ya mwandishi (Msokile, 1992). Uchunguzi wa mtindo kwa hivyo, unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati na tamathali za usemi. Uchanganuzi wa mitindo ya lugha umeongozwa na mhimili wa nadharia ya umitindo inayoonyesha kwamba lugha tumizi humtambulisha mhusika. Wasomaji na wahakiki wa fasihi hutegemea lugha, mienendo na tabia za wahusika kuwaelewa kupitia matumizi ya mbinu kadhaa kama vile mbinu ya kimaelezi, kidrama na mbinu rejeshi. Imebainika kuwa mienendo na lugha za wahusika wazimu haziwezi kutumika kudhihirisha hulka zao kwa sababu kisaikolojia hawana akili razini. Kwa hivyo mara nyingi maelezo ya mwandishi hutumiwa kuwabainisha wahusika hao.

**Maelezo ya Mwandishi**

Mwandishi Habwe amewabainisha wahusika wazimu kupitia maelezo. Katika mbinu hii mwandishi badala ya kuwaacha wahusika wajieleze au watambulikane kwa matendo yao huzieleza sifa zao. Derrida (1978) katika (Veit-Weild, 2006) anasema kuwa lugha kama (usemi) na wazimu kama (ukimya) zimetengana na kwamba wazimu unaweza kuelezwa katika lugha ya ubunifu.

Katika kitabu cha *Paradiso* tunapata maelezo ya msimulizi akisema kuhusu familia ya mama ya Patricia:

> *Jumla ya watoto walikuwa kumi. Watatu walifariki dunia. Wawili ni wazimu. Wawili wamepotea sasa miaka ishirini hawarudi nyumbani. Wamebakiwa na huyu mmoja tu Patricia ambaye maisha nayo yamemwendea upogo”* (uk 191).

Mhimili kuu wa nadharia ya umitindo ni kuwa lugha tumizi humtambulisha mhusika. Hapa tunapata kuarifiwa kuhusu hali ya familia bila wao kusema chochote wala sababu ya wazimu wao kuelezwa. Msanii alitumia mbinu hii katika sehemu kadhaa ya kazi zake. Tunapata maelezo kama hayo pia katika *Fumbo La Maisha*:

> *Watoto wazima walikimbilia usalama kwa jirani walipoona mama amechukua bunduki ya baba anatisha kuwapiga risasi wote. ‘Tafadhali, tafadhali’, baba watoto aliomba na kumbembeleza mkewe aliyegeuka wazimu kwa kusikia mume anafanya dharau ya kufanya mapenzi. Mama alizungusha Doko nyumba nzima akiwa uchi. Hatimaye Doko alitoka na chupi. Susan alishuka mori… Susan ni kama alikuwa na pande mbili, upande wa uzima na upande wa wehu. Alimfuata huyo mpenzi wa mumewe akamzomea na kumpa vitisho* (uk 46).

Tunaarifiwa kuhusu hali ya Susan na kuelezwa matendo yake na msimulizi. Katika kisa hiki matendo ya Susan yaliyoelezwa na msimulizi ndiyo yanamtambulisha kama wazimu.

Kwingine katika kitabu hicho tunaelezwa wazimu wa Ali; sababu na athari yake:

> *Ali alikaa na jamaa yake mjini Mombasa Amu yake naye alikuwa mkwezi akipanda minazi kwa matumizi. Ami ya Ali alitumia dawa za kulevya zikamtia wazimu. Mkewe, Bi Sabina akamtoroka akabaki na Ali. Kazi yake ya ukwezi akaiacha na kujizungukia mabarabarani* (uk 90).

Tunamtambua Ali kama wazimu kutokana na maelezo ya mwandishi. Mbinu ya maelezo ni mbinu ambapo msimulizi anaweza kuelezea wasifu wa mhusika, msukumo wa matendo yake, mazingira yake na amali zake ili msomaji auone mtazamo huo (Murumba, 2013). Lugha tumizi umemtambulisha mhusika. Pamoja na kuelewa hali ya wazimu wake tunaelewa pia hali yake ya umasikini. Kwa kutumia mbinu ya kimaelezi mwandishi Habwe amewabainisha wahusika wazimu katika visa vyote vilivyochanganuliwa katika riwaya teule katika kazi hii.

Katika *Safari ya Lamu* Tunasoma kuwa :

> *Hapo kulikuwa pia na wendawazimu wawili mmoja alikuwa mwanamume ambaye alikuwa uchi kama hayawani. Mwanamke ndiye*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

> *aliyefunga kipande cha leso ambacho hakikumsitiri… kipande kiliacha matiti na tumbo lake wazi. Mwanamke alionekana kama aliyekuwa mzima siku si nyingi zilizopita* (uk 52).

Maelezo tunayoyapata hapa kuhusu mavazi yanawatambulisha wazimu hawa. Katika tukio hili maneno ya mhusika mwanamke hayaonyeshi akili iliyovurugwa isipokuwa anapotaja nguo zake zinazotokea Dubai:

> *Unaona huna nguo. Huwezi kununua nguo. Sasa nguo yangu yatoka Dubai utaweza?* (uk 53).

Lugha iliyotumiwa na mwandishi inawabainisha hao wazimu na kwa yule anayemwona huyu mwanamke ataelewa kuwa maneno yake hayaoani na hali yake.

Katika *Safari ya Lamu* pia tunapata maelezo kuhusu familia ya mhusika mwingine. Mama wa Yankee alishikwa na wazimu na kwamba alikuwa akizungumza mambo yasiyoeleweka. Maelezo hayo yanatufanya kumbainisha kama wazimu:

> *Watu walikuwa wakisema aliiba pesa za mhindi naye mhindi akamwombea dua mbaya. Watoto wa baba yake Yankee walishikwa na maradhi. Wengi kama Yankee hawangeweza kusoma chochote darasani, majini na mashetani yaliwasumbua … mama wa mji huo alishikwa na wazimu. Alizungumza mambo yasiyoeleweka* (uk 117).

Kupitia kwa maelezo hayo, wizi wa mali ya mhindi umesababisha wazimu wa mke wa Mwamba. Hatumwoni mke huyu akitenda wala kutagusana na wahusika wengine. Hata hivyo tumemtambua kupitia masimulizi

Mwandishi ameendelea kuwatambulisha wahusika wazimu katika kitabu cha *Kovu Moyoni* akiandika hivi kuhusu Mwalimu Katuku :

> *Walimjia usiku huo wakawatendea familia yake vitendo vya kikatili. Hawakumchukulia chochote. Katuku alishikwa na wazimu kwa ajili ya hivyo visa vya jana… alipotea nyumbani hakuna aliyejua aliko hadi sasa. Alipoonekana mara ya mwisho alikuwa akijisemesha huku akirusha mikono kama punguani* (uk 54).

Hapa tunaarifiwa kisa kilichopelekea yeye kushikwa na wazimu pamoja na matendo ya kiwazimu anayoyatenda. Maelezo kama haya tunapata pia kuhusu mhusika Jumaa Mambo ambaye alihusika katika kutesa watu. Wahusika wawili Eddah na Nilfreda wakikumbuka matukio ya awali tunaarifiwa kuwa:

> *Kwa muda walikaa pale mwembeni wakikaa wakicheka. Walipata nafasi ya kurudi katika mateso ya nyuma. Waliyajadili, yakiwaudhi, yakiwakera, yakiwaliwaza. 'Yuko vipi, Mambo?' Eddah aliuliza ... Mambo ni kama maisha yamemwendea segemnege. Ameshikwa na wazimu* (uk 127).

Kupitia kwa wahusika hao wawili tunajua kuwa mhusika Mambo ni wazimu. Katika ukurasa mwingine tunaarifiwa kuhusu wazimu wa Boke mamake Mwita:

> *Tangu Mwita alipohukumiwa na hatimaye kunyongwa Boke ni kama alishikwa na wazimu. Alitembelea matambara. Eddah na Mulota walimsihi atulie, lakini hakusikiliza lolote* (uk 133).

Katika kisa hiki tumearifiwa kuwa Boke ni wazimu na sababu ni kunyongwa kwa mtoto wake.

Aidha mwandishi amewabainisha wahusika wazimu kupitia masimulizi ya matendo na mahusiano yao na wahusika wengine.. Ingawa Wamitila (2008, uk. 172) anadai kwamba maelezo ya mhusika mmoja kumhusu mwingine huenda yasitegemewe hasa kwa vile maelezo hayo huenda yakaathiriwa na mtazamo wa mhusika binafsi, mwandishi Habwe ametumia mbinu hii kuwabainisha wahusika wazimu. Maelezo hayo yametolewa na mhusika mmoja kumhusu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

mhusika mwingine katika *Safari ya lamu.* Mwandishi sasa ameeleza juu ya maisha ya mhusika katika familia kupitia kwa msimulizi ambaye ni ndugu ya mwathiriwa. Asema:

> *"Ndugu yetu mmoja tu, Simba, ndiye aliyesoma hadi kupita vizuri na kujiunga na chuo kikuu cha Egerton. Baada ya kupata shahada, miaka kumi imepita hajapata kazi. Anaishi kwa kuomba. Siku yoyote atarukwa na akili kwa mawazo. Haogi, tena manywele yamemtoka na ndevu*" ( uk 71).

Maelezo ya mwathiriwa huyu yanaendelea katika uk 90.

> *"Akili zangu zilimkumbuka kaka yangu ambaye alikuwa akiumwa. Habari za kuugua kwake zingeweza kumtia mama wazimu akawa kama yeye. Habari nilizopata ni kuwa sasa amepotea hawajui yuko wapi. Alikula mapipani. Alitembea uchi na kulala katika baridi ya usiku. Daktari ametuambia ni mawazo yaliyosababisha hiyo hali yake …"*

Mwandishi anakamilisha maelezo yake kuhusu mhusika Simba katika uk 201:

> *"mama tayari alisetwa na mawazo ya ndugu yangu ambaye sasa ameshikwa na wazimu ndugu yangu alizunguka mabarabarani. Alilala porini bila chakula wala kipande cha blanketi…"*

Katika kisa hiki mwandishi anatujuvya hali ya mhusika kupitia maelezo ya jamaa yake. Kwa njia hiyo tunathibitisha kuwa mhusika Simba ni wazimu.

Mazungumzo ya wahusika wenyewe pia yametumiwa kuashiria upungufu wa kiakili. Mhusika mwengine azungumze na mwenzake na kumwita wazimu katika kitabu cha *Safari ya Lamu*.

> *Mwandishi asema: "Utanitambua leo", alimweleza huyo babu aliyejaribu kutoroka. Mama alikuwa ameshika jiwe…"Baasi", huyo bwana aliomba msamaha. "Baasi mamako. Usinichezee wewe wazimu. Mwaiba vitu vya watu mkishaletewa majini yawatia wazimu"* (uk 52).

Murumba (2013) katika tahakiki yake ya 'Mtindo katika *Watu wa Gehena',* anauita mtindo wa 'kidrama' ambapo msanii anawaonyesha wahusika wakitenda matendo na kuzungumza. Kwa kuzingatia nadharia ya umitindo, lugha iliyotumiwa hapa imewatambulisha wahusika kuwa wazimu. Milner (1987) anaeleza wazimu kama hali ambapo mwathiriwa ametengwa na uhalisia kiasi cha kutoweza kuelewa maana sawa na watu wengine wala kuathirika nayo. Wazimu wawili wanasemezana huku mmoja anamwita mwenzake wazimu. Wote ni uchi wala hawajaathiriwa na hali yao:

> *'ambaye alikuwa uchi kama hayawani. Mwanamke ndiye aliyefunga kipande cha leso ambacho hakikumsitiri… kipande kiliacha matiti na tumbo lake wazi*' (uk 52).

Mwandishi amewabainisha kama wazimu kwa kueleza matendo na maneno hayo wakiwa katika hali hii.

**Tamathali za Usemi**

Msanii hutumia tamathali za usemi ili aweze kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Mwamanda (2008) anaona tamathali za semi kama viwakilisho au vifananisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti zinazofanana. Kwamba zinabadilisha maana dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya fasihi iliyokususudiwa na msanii.

Katika sehemu hii, tamathali za usemi imetumiwa kwa maana ya: maneno, nahau au sentensi iliyotumiwa kwa njia ya kipekee ili kuwakilisha maana nyingine tofauti na ile iliyozoelewa ya matumizi ya kawaida ya lugha. Mafungu matatu yanadhihirika za tamathali za semi kwa mujibu wa Maumulla (2009) : tamathali za mafumbo, tamathali za mlinganisho na tamathali za msisitizo. Tamathali za mafumbo ni kama dhihaka, tasfida,

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

stihizai/kejeli/kinaya na kidahizo. Za mlinganisho ni sitiari, tashbiha, tashihisi, taashira, taniaba na majazi. Nazo za msisitizo ni mubaalagha, metonumia na ritifaa. Katika kazi hii mbinu zifuatazo zimeshughuikiwa: Sitiari, Tabaini, Misemo, Ritifaa, Uzungumzi nafsia, Tashbihi, Taswira, Mbinu rejeshi na Maswali balagha. Kazi hii imeangaza jinsi tamathali za usemi zilivyotumiwa kuwabainisha wahusika wazimu katika kazi teule za Habwe.

***Sitiari***

Kwa mujibu wa Kamusi Elezi ya Kiswahili (Chiduo, 2016), sitiari ni tamathali ya semi inayotumika kulinganisha vitu au kitu kimoja na kingine chenye sifa zinazokaribiana nacho moja kwa moja. Ni mbinu ya ulinganishi wa moja kwa moja ambapo kitu fulani kinapewa sifa za kitu kingine bila kutumia viungio vya kulinganisha kama mithili ya, kwa mfano, ja, na kama (Wamitila, 2003).

Mbinu hii haikutumika kwa wingi katika kazi za Habwe ambazo zilichunguzwa. Na ilipotumika ilitambulisha msemaji kama ni wazimu. Katika riwaya ya *Paradiso,* mhusika Musa anawaita Joshua na mkewe Lona, 'shetani'. Maneno hayo yanafanya Joshua kughutuka na kuelewa kuwa hali ya Joshua ni mbaya sasa. Gelder (2001) akiorodhesha aina za wazimu anataja ile ya kuathiri mfumo wa neva unaotokana na mfadhaiko. Musa amebadilika pole pole toka kuwa mhubiri mwenza wa kina Joshua. Sasa anaweza kuwakabili wahubiri na kuwaita shetani hadharani na mchana peupe. Kupitia mhusika Musa mwandishi anasema:

> *"Nyinyi ni shetani! Ati wahubiri? Wahubiri gani nyinyi? Nyinyi ni laghai…? (uk 75)*.

Mhusika Musa anawalinganisha Joshua na mkewe na shetani. Matumizi ya istiari hapa inawafanya wengine watambua wazimu wa Musa kwa sababu kwa kawadia hangewashambulia waumini viongozi wa kanisa kwa njia hiyo. Fikra ya maneno ya Musa yalimjia tena Joshua. Mwandishi anasema:

> *Alisimama akaanza kutembea ugani. Hapo ndipo maneno ya Musa yalipomjia. Mara ile alidhani Musa ni mwendawazimu* (uk 103).

Sitiari jinsi ilivyoelezwa na Wamitila (2003) kama mbinu ya ulinganishi wa moja kwa moja, imetumiwa kubainisha mhusika Musa kama wazimu. Lugha tumizi humtambulisha mhusika tukizingati nadharia ya umitindo (Leech, 1969).

***Tabaini***

Hii ni aina ya tamathali ya msisitizo lakini msisitizo huu hujitokeza kwa mtindo wa kinyume. Tabaini huonyeshwa kwa matumizi ya 'si' ya kukanusha. Husisitiza jambo kwa kutumia maneno yasiyoonyesha msisitizo huo waziwazi (Wamitila, 2003). Mifano: Si hayati si mamati, si mgonjwa si mzima, si midukuo hiyo si matusi hayo**.** Habwe ametumia mbinu hii kama njia mojawapo ya kuwabainisha wahusika wazimu. Katika riwaya ya *Safari ya Lamu* mwandishi anaonyesha hali ya maisha ya akina Simba na Musa. Msimulizi anahesabu vitu amabavyo mama yao alidaiwa. Kupitia masimulizi hayo, wasomaji wanaweza kukadiria kiwango cha umasikini. Ni kiwango hicho cha umaskini kinachopelekea Simba kuwa wazimu. Anasema:

> *"Pesa hizo hazikutosha kulipia madeni, karo, kutuvisha wala kutulisha. Mama alidaiwa chumvi, kama si sukari. Alidaiwa majani ya chai kama si maziwa. Alidaiwa unga wa dona kama si mafuta ya kijiko… Ndugu yetu mmoja tu, Simba ndiye aliyesoma… Baada ya kupata shahada, miaka kumi imepita hajapata kazi… Anaishi kwa kuomba. Amevunjikiwa. Siku yoyote atarukwa na akili kwa mawazo*" (Uk 71).

Kupitia kwa mbinu hii ya tabaini tunajuvya hali ambayo inahofiwa kuwa ingesababisha wazimu kwa Simba baadaye. Nadharia ya Umitindo hurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani kwa lengo mahususi. Lengo la mwandishi ni kutujuvya masaibu ya familia hii ili tumwelewe mhusika Simba. Nadharia ya uhalisia wa kijamaa inahusu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

maelezo ya hali halisi ya kibinadamu ya kiuchumi miongoni mwa hali nyingine. Lugha katika nadharia ya uhalisia hulitambulisha tabaka (Madumulla, 2009) Aidha kwa vile lugha tumizi humtambulisha mhusika, familia ya Simba ambaye ni wazimu ni wachochole. Hali hii pia imeendelezwa na vijana waliosoma na kisha kukosa kazi na mahitaji muhimu katika maisha.

***Misemo***

Msemo ni fungu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu kwa namna maalum ili kutoa maadili (Tuki, 2014). Ni kauli fupifupi zinazotumiwa na jamii ili kusisitiza ukweli wa jambo au kutoa msisitizo wa maadili fulani. Huunganisha dhana au mawazo mawili kuwa moja. Rono (2013), katika kushughulikia uhakiki wa kifani na kimaudhui wa riwaya ya Kidagaa Kimemwozea, aliorodhesha msemo kama mbinu mojawapo ya kudhihirisha hulka za wahusika. Murungi (2013) ameonyesha jinsi mbinu za lugha na mbinu za sanaa zinavyoweza kufanikisha malengo ya msanii. Kazi yake pia ilionyesha jinsi mitindo ilivyotumiwa kudhihirisha ngazi za maisha ya wahusika na mwonoulimwengu wao. Msemo kama mbinu unaweza kutumiwa kuonyesha hali ya maisha ya mhusika na kuchangia kuwabainisha. Katika uchunguzi huu, Habwe ametumia misemo katika visa vichache kubaini wazimu.

Katika *Safari ya Lamu* msimulizi anasema:

> *"Kila mja ni wake maulana hata yule anayeonekana duni sana. Ndio sababu yule wazimu yuko pale mwembeni anakula taka, anakula masazo lakini hafi…"* (uk 177).

Sanaa ya kiuhalisia ni ile iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka (Ntarangwi 2004). Msemo huu unabainisha wazimu bila kutajwa jina. Mwanzo unatuonyesha maisha ya wachochole ambao hutegemea Maulana na wanaoonekana duni. Kisha baada ya kutaja wazimu ameendelea kueleza matendo ya kiwazimu kama vile kula taka na masazo. Kwa njia hii amewabainisha wazimu.

Katika kitabu cha *Kovu Moyoni* na kupitia wahusika Edda na Nilfreda mwandishi anaeleza:

> *"Ee anasema nyuki wanamfuata pia… "Nyuki kwa kweli au ni wazimu?"… mabaya yatalipwa hapa hapa duniani"* (uk 127).

Wakimrejelea Jumaa Mambo ambaye amekuwa wazimu kwa sababu ya unyama aliyowatendea watu awali. Edda anasema kuwa mabaya yatalipwa hapa hapa duniani. Kutokana na maoni yake tunachukulia kuwa wazimu wa Mambo umesababishwa na matendo yake mabaya kwa watu kwamba Mungu anamwadhibu. Pia mwandishi ametumia segemnege:

> *"Mambo misha ni kama yamemwendea segemnege. Ameshikwa na wazimu". (uk 127 )*

Kumaanisha maisha ya Jumaa Mambo yameharibika. Katika kisehemu hiki tumedhihirisha jinsi msemo ulivyotumiwa na msanii Habwe kuwabainisha wahusika wazimu kwa kutumia nadharia ya umitindo kama dira ya kuchanganua data.

***Ritifaa***

Kahigi (1994) anadai kuwa kanuni ya jumla ya uhamishaji wa maana ya kitamathali inachukua nafasi ya maana ya kawaida. Katika uwanja wa fasihi ritifaa hutumiwa kurejelea mbinu ambapo mhusika husema na mhusika asiyekuwepo (Chiduo et al, 2016 Ni mbinu ya kuzungumza na mtu au kitu kisichokuwepo, kumsemesha mfu au mhusika ambaye ametoweka kana kwamba yuko pamoja nawe.

Nyakati za mwandishi Shakespeare wahusika walio na hatia ya kuwaua wengine walichorwa mara nyingi wakionyesha athari ya matendo yao maovu ikiwa ni pamoja na kuongea na watu wasiokuwepo. Nazemi na wengine (2020), akinukuu Ross, D. W (1989) anaeleza jinsi mhusika Macbeth katika tamthilia ya Shakepeare *Macbeth* alivyoathirika na kitendo cha kuhusika katika mauaji ya mfalme ambaye alikuwa binamu ya bwana yake. Nazemi anatupa taswira ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

mgonjwa wa kiakili: anatembea akilala na kuongea na watu wasioonekana juu ya matendo yake. Pia tunaarifiwa kuwa kila mara ananawa mikono katika juhudi za kuitakasa kutokana na damu za wale aliowaua. Katika historia ya fasihi waandishi wamechora wahusika wenye akili razini wanaoongea na wafu katika harakati za kuomboleza. Vilevile wahusika wazimu wamechorwa wakiongea na wale waliokufa na kuwaaminisha wanajamii kuwa ni ishara kuwa waathiriwa walihusika katika mauaji.

Habwe ametumia mbinu hii kumbainisha mhusika wazimu kupitia mhusika Dora katika kitabu cha *Fumbo la Maisha*. Anasema:

> *"Ah! Husna sitaki mchezo wako mimi ni mamako. Tafadhali! Tafadhali! Husna usinigonge kwa gari Husna!" 'Tulishangaa huyu bibi alivyogombana na mtu aliyekufa tayari…Dora aliendelea na vitimbi vyake. Selume alishauri apelekwe hospitali ya wagonjwa wa akili'* (uk 157).

Katika hali yake ya wazimu Dora anamwona marehemu Husna ambaye inasemekana kuwa yeye alihusika katika kifo chake. Jambo hili linafanya wazo kuwa wazimu wake umetokana na ushirikina uliokatisha maisha ya Husna kuwa na mashiko na vile vile kuthibitisha kuwa matumizi ya ritifaa yamebainisha Dora kuwa wazimu

***Uzungumzi Nafsia***

Katika tamathali hii mhusika hujizungumzia, ama kwa kuongea au kuwaza, bila kukusudia kusikika na yeyote. Ni maongezi marefu yanayotolewa na mhusika mmoja yenye dhamira ya kuukuza msuko. Uzungumzi nafsi wa ndani hurejelea kifungu kinachomulika mawazo yanayompitikia mhusika fulani akilini (Wamitila, 2003).

Habwe ametumia mbinu hii kuwabainisha wazimu katika kazi zake mbili zifuatavyo:

Katika *Fumbo la maisha*, anasema:

> *Picha ya Dora ilimpitikia akilini. "Dora ndiye aliyekuwa mtu wa bei pale majengo. Imekuwaje amekuwa kama kinyesi? Kwa nini binadamu anazaliwa katika masumbuko yale?… Lakini kama ni Dora aliyemfanyia Husna dawa, alipaswa kuteseka anavyoteseka, maana Husna angebadili mkimbio wa maisha yangu …"* (uk 178).

Kupitia kwa uzungumzi nafsia wa mhusika huyu tunathibitisha kuwa Dora ni wazimu. Aidha tunaelewa kisababishi cha wazimu wake (kufanyia Husna dawa) na hisia za Mwanaisha (mamake Husna) kuhusu hali yake hiyo. Maelezo pia yanadhihirisha hali ya uchochole ambayo ndiyo nguzo muhimu katika maandishi ya kiuhalisia.

Katika kitabu cha *Kovu Moyoni* mwandishi asema:

> *Mwalimu Katuku alipoonekana mara ya mwisho alikuwa akijisemesha huku akirusha mikono kama punguani. Maneno aliyoyasema ilikuwa vigumu kuyaelewa lakini ni kama alisikika akisema, "Maisha! Life ! Maisha! Life ! Bure kabisa"*(uk 54 na 55).

Kujisemea kwake hapa ni kuonyesha amerukwa na akili akisaka maana ya maisha. Anashinda akirudia maneno hayo asichoke. Nadharia ya umitindo inasema kuwa lugha tumizi humtambulisha mhusika. Ni rahisi kutambua mja anayesema peke yake na hasa ikiwa maneno yake hayaleti maana kwa wanaosikiliza. Kwa mbinu hii msanii amemtambulisha Katuku kama wazimu.

***Tashbihi***

Tashbihi ni tamathali ya usemi wa ufananisho au mlinganisho wa vitu viwili ambapo vitu hivyo viwili hulinganishwa kwa njia ya waziwazi kwa kutumia maneno ya kulinganisha; 'kama', 'mithili ya', 'sawa na', 'ja'. Lugwiri (2011) aliyetumia nadharia ya umitindo katika kushughulikia Sitiari, Taashira na Tashbiha katika *Utenzi wa Tambuka* anabainisha wazi jinsi vipengele vya tamathali za usemi vinavyoweza kutumika kufikia malengo ya utafiti.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Mwandishi Habwe ametumia mbinu hii kufananisha hali na matendo ya wahusika fulani na wazimu.

Katika *Cheche za Moto* mwandishi anasema:

> *"Sasa Dole alirudi nyumbani Buda baada ya kufutwa kazi jeshini… hana chakula, hana mke, hana mtoto, hana nyumba. Anajizungukia Buda akitafuta msaada. Ni kama wazimu hasa. Ni kama alikaa katika sayari yake*" (uk 159).

Matendo ya Dole na hali yake hapa yamelinganishwa na yale ya wazimu na kutumiwa kuyabaini wazimu. Vile vile kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa maelezo ya maisha duni na ya akina yakhe yametumiwa. Lugha tumizi imewabainisha kulingana na nadharia ya umitindo.

Riwaya ya *Paradiso* ina wahusika wawili familia moja ambao mwandishi ametuwasilishia. Kupitia mhusika Amuko mwenyewe mwandishi anasema:

> *"Mimi nina shida na mwanangu. Ameshikwa na magonjwa kiasi cha kuwa kama wazimu. Hiyo ni baada ya kuishi na mamake akiwa katika hali hiyo hiyo ya wazimu. Mama amekuwa katika hali hiyo miaka kumi. Hataki kusema. Hataki kula. Amekuwa mithili ya zuzu tu"* (uk 40).

Katika kisa hiki kuna wazimu wawili mama na mtoto. Tunawatambua kupitia maelezo ya msimulizi anayetumia mbinu ya tashbihi. Hali ya mtoto ndiyo inayolinganishwa na mama ambaye amekuwa mgonjwa kwa muongo mmoja. Ukimya hapa ni ishara ya kuwa mgonjwa wa kiakili Nazemi (2022)

***Taswira***

Taswira hurejelea kirai au maelezo yanayounda picha fulani katika akili ya msomaji. Wamitila (2003) amefafanua matapo mawili makuu ya taswira: ishara na maelezo. Akichanganua zaidi taswira za maelezo, anaibuka na baadhi yavyo kama taswira za uoni, za mguso, za mwonjo na usikivu. Taswira zote hizo zinajitokeza kupitia maelezo ya mwandishi. Kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya umitindo ambayo ni kuwa lugha tumizi humtambulisha mhusika, Habwe ametumia taswira kuwabainisha wahusika wazimu.

Senkoro (1982) anayaweka taswira hizo katika makundi matatu makuu: taswira zionekanazo, za mawazo na hisi. Taswira za hisi huibua hisi fulani mawazoni na kushughulikia mielekeo ya kihisia ya msomaji kuhusu hali fulani. Nadharia ya Uhalisia wa kijamaa ina mhimili wake mmoja unasema kuwa: wahusika katika fasihi hutumiwa kupinga dhulma (Flores, 2014). Msanii ametumia mbinu ya taswira kujieleza. Taswira zina nguvu kubwa ya kuganda akilini na kumwezesha msomaji kuupata ujumbe wa mtunzi vizuri (Senkoro, 1982). Katika sehemu hii tumedhihirisha jinsi mwandishi ametumia mbinu ya taswira kuwabainisha wazimu na hivyo kufikia madhumuni ya utafiti.

Katika *Paradiso* tunapata maelezo kuhusu hali ya mama Julia:

> *"Mwaka mmoja mbele mama Julia amefanyiwa dawa akashikwa na wazimu. Leo anazuru mitaa ya Mombasa. Asubuhi yuko Miritini. Mchana utamkuta Mtwapa kazi yake kubwa anakusanya karatasi na kuhubiri hadharani*" (uk 61).

Hapo tunapata picha ya wazimu kwa maelezo ya hali na matendo yake mama Julia. Mbili kati ya taswira zilizoorodheshwa na Wamitila (2003) zinajitokeza hapa: za uoni na za usikivu. Taswira ya mtu anayezuzurura mitaa na hasa matendo ya kusanya karatasi inayochorwa hapa inabaini mhusika wazimu. Milner (1987) anaeleza wazimu kuwa hali ambapo mwathiriwa ametengwa na uhalisia asiweze kuelewa maana sawa na watu wengine wala kuathirika nayo. Anatoa mfano wa mwathiriwa kuzurura mitaa akiokota vitu vingine kwenye jalala la taka na kubeba kama mzigo wake.

Mhusika mwengine Musa katika *Paradiso* pia amebainishwa kwa taswira kama hizi:

> *"Leo alionekana barabarani akiyazungukia.*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

> *Ameshikwa na wazimu yuwaenda mithili ya bahaimu wa maporini hasa! … Baadaye mama mmoja Julie akasema amemwona Musa karibu na kituo cha basi cha Ambassadeur akiokota karatasi huku amerarukiwa… Baadaye Joshua alikuwa ametoka kutafuta vifaa vya kanisa wakifuatana na Lona. Alisimama kama bubu akamtazama Musa na sarakasi yake ya karatasi za plastiki. Musa alikuwa akicheza densi hasa… Mate yalimdondoka. Lona hakuamini ambavyo Musa alikuwa amevaa mavazi yaliyomweka matako wazi"* (uk 74)

Katika kisa hiki taswira zinadhihirisha hali ya wazimu kuzingatia mavazi na matendo na hivyo kumbainisha mhusika wazimu (Milner, 1987).

Taswira hizi zinaendelea kutumika katika *Fumbo la Maisha* msanii anaposema:

> *"Dora aliamka kila siku akaanza kuzunguka barabara huku amevaa karatasi ya nailoni kichwani. Hakuvaa chochote miguuni. Amevaa nguo kiajabu. Mkononi alishika kitu alichokiita gari. Alipokuwa akikimbia aliguruma kama gari Ndruuuuu!"* (uk 157).

Maelezo ya matendo na mavazi hapa yanachora taswira ya wazimu (Milner, 1987)

Makundi matatu makuu ya taswira kwa mujibu wa Senkoro (keshatajwa) ni: zionekanazo, za mawazo, na hisi. Alieleza taswira za mawazo kama za kidhahania, ilhali taswira za hisi huibua hisi fulani mawazoni. Taswira za mawazo na hisi ndizo zimetumiwa na mwandishi katika visa hivi kuwatambulisha wazimu.

Katika *Cheche za mtoto* mwandishi anasema:

> *"Mareal alikuwa amegeuka zuzu la udenda lisilosema vizuri wala lisilowaza kwa urazini… Mareal hakuweza kujibu wala hakushugulika na watu waliomdhiki kwa maswali. Hakutaka kukaa na watu pale nyumbani. Akiona watu hujificha* (uk 42 na 43).

Pia asema kuhusu mhusika mwengine mwathiriwa wa kifo cha mtoto wake:

> *"Mamake Muga mpaka leo ni mahoka, hasikii, haoni, hali. Anaimba nyimbo ambazo hazieleweki"* (uk 169).

Maelezo ya matendo yake yanamtambulisha mamake Muga kama wazimu tukizingatia maelezo ya Milner (1987) na Olson (2014) kuhusu dalili ya wazimu.

Katika *Safari ya Lamu* msimulizi anaeleza hali ya ndugu yake:

> *"Habari za kuuugua kwake zingeweza kumtia mama wazimu akawa kama yeye… Sasa amepotea hawajui yuko wapi. Alikula mapipani. Alitembea uchi alilala katika baridi ya usiku…"* (uk 90).

> *"Ndugu alizunguka mabarabarani. Alilala porini bila chakula wala hata kipande cha blanketi"* (uk 201).

Olson (2014) anaeleza dalili nyingine ya mgonjwa wa kiakili wa kutotaka kulala ndani ya nyumba na kutembea uchi. Kuhusu ndugu ya Musa, Simba tunaona taswira ya wazimu kweli; kutembea uchi, kuzunguka, kulala porini na Habwe ametumia taswira hizi kumbainisha mhusika huyu.

Taswira za mja ambaye anasumbuka kiakili pia zinajitokeza katika *Kovu Moyoni*:

> *"Nyuma yake aliona mtu anakuja kwa kasi hali amevaa matambara. Kichwani alitia kaptula kama kofia. Kaptula hii ikafanya ugumu wa kumtambua… 'Ua! Ua! Ua! Tuum trum! Nyuki! Nyuki! Nyuki!' Alilia huyo mtu akiwinga nyuki*" (uk 108).

Picha hii ni ya mtu ambaye amesumbuliwa sana kiakili (Ross, 1989). Imetumiwa kudhihirisha wazimu. Mwandishi Habwe ametumia taswira za uoni, usikivu, na hisi miongoni mwa nyingine kuwabainisha wazimu. Kwa mujibu wa mhimili wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

nadharia ya umitindo kuwa lugha tumizi humtambulisha mhusika, ameeleza mavazi, maongezi na matendo kwa njia ambayo inawabainisha wahusika wazimu

***Mbinu Rejeshi***

Wamitila (2003) anaeleza mbinu rejeshi kuwa mbinu ya uhusika ambapo mwandishi anazielezea sifa za wahusika wake badala ya kuwaacha watambulikane kutokana na matendo yao. Nadharia ya umitindo inaeleza kuwa lugha tumizi humtambulisha mhusika (Leech, 1969). Mbinu rejeshi inayoelezea matukio yaliyotokea wakati wa nyuma ya hadithi imetumiwa na Habwe kubainisha wahusika wazimu. Katika riwaya ya *Paradiso* anaeleza visababishi vya kijumla vya wazimu bila kutaja mhusika mahsusi. Anasema:

> *"Pia karibu nao kulikuwa na Mohamed Mazoa ambaye alikuwa amefuga majini…Haya majini yalihangaisha watu mwezi mmoja yakiwaomba hiki na kile. Wakati mwingine majini hayo walijigeuza wasichana na yakaghilibu vijana wakaenda wakalala nayo bila kujua. Hao vijana walizuzuka vichwa wakawa wazimu…*" (uk 13-14).

Kwa kutumia mbinu rejeshi mwandishi amewabainisha wazimu. Gelder (2001) akiorodhesha visababishi vya hali za wazimu, anataja athari ya dawa za kulevya na ushirikina ambazo huleta mfadhaiko wa kiakili. Vijana waliozuzuka wanaweza kubainishwa kuwa wazimu bila kuangalia mavazi wala matendo.

Kwingine mbinu hii inatuwezesha kuelewa kuwa kabla ya Amuko kuja kanisani kuombewa amekuwa na mtoto na mama wagonjwa wa kiakili ambao wazimu wao ulitokana na matendo maovu ya awali ya Amuko. Anasema katika riwaya ya *Paradiso:*

> *"Hiyo ni baada ya kuishi na mamake akiwa katika hali hiyo hiyo ya wazimu. Mama amekuwa katika hali hiyo miaka kumi."…. Michael aliendelea kuomba huku akipewa maono ya Amuko. Ombi hilo lilizidi kumliza Amuko ambaye tayari alikubali kuwa alipokuwa akiishi Italia alihadaiwa kufanya kafara ili apate mali"* (uk 40 na 41).

Katika kisa hiki wahusika wazimu wamebainishwa kwa kutumia mbinu rejeshi na kwa hivyo madhumuni ya utafiti kufikiwa.

Katika *Paradiso* pia mwandishi asema:

> *"Habari za Musa zilipofika pale New Jerusalem hakuna aliyetaka kuzitamka… masaibu mengi yalimkumba. Tapeli mmoja alimtapeli katika biashara yake ya zebaki. Baadaye mtoto wake alimwibia bumba la pesa. Leo alionekana barabarani akiyazungukia. Ameshikwa na wazimu*" (Uk 74).

Hapa mbinu rejeshi imetumiwa kuonyesha maisha ya Musa kabla ya yeye kuwa wazimu. Matukio haya ya awali yamechangia hali yake ya wazimu. Kwa hivyo mbinu rejeshi inambainisha.

Mhusika mwengine amekumbuka maisha ya awali ya Musa. Hapa tunarejeshwa katika tukio zima la maisha ya Musa likiangaliwa na Rose ambaye pia ni mwathiriwa:

> *"Rose alimshuhudia Musa kuingia kanisani na baadaye kuacha na kuingia katika biashara. Musa aliposhikwa na wazimu baada ya kuwa mfilisi ni mambo yaliyomshangaza sana Rose. Hata hivyo Rose alielewa kuwa Mungu wa Israeli pamoja na kuwa mwenye huruma alikuwa pia Mungu wa hasira… si ajabu Musa aliadhibiwa*" (uk 106).

Mbinu rejeshi hii inambainisha Musa kama wazimu

Mhusika Nandi katika *Cheche za* Moto anakumbuka maovu yake ya awali yaliyopelekea mamake Muga kuwa wazimu:

> *"Baba nimekosa unisamehe na uniokoe… Alisema taratibu huku magoti yakialika na akajitupa kitandani. Hata kitandani alikumbuka*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

> *kifo cha Muga. Mamake Muga mpaka leo ni mahoka… Kisa na maana ni mwanawe. Nandi alishusha pumzi*" (uk 169).

Mbinu rejeshi imetumiwa kutujuvya matukio ya awali yaliyopelekea kuuawa kwa Muga na athari ya kifo chake kuangaliwa kama kisababishi cha wazimu wa mamake. Hapa mhusika anayetambulishwa na mbinu rejeshi hii ni mamake Muga ambaye pia ni jamaa ya kina Nandi.

Katika *Fumbo la maisha* mwandishi ametupa maisha ya awali ya Dora katika familia ikianza na babu yake Mtori, mamake Subira na Dora mwenyewe akieleza sababu ya wazimu:

> *"Dora, maskini, alipozunguka barabarani nilikumbuka kadhia yake. Babu yake Mtori alikuwa mmoja katika wapiganiaji wa Mau Mau… Mkewe mtori alimwacha na watoto wawili Subira na Herman baada ya ndugu yake kumnyanganya shamba lake kortini… Subira alitoka siku moja akaenda kumwona babake ambaye sasa amekuwa wazimu… Hiyo ndiyo sababu iliyompa Subira kuingia majengo na hata Dora…*" (uk 160, 162, 163)

Wamitila (2008) anasema kuwa msanii ana uhuru wa kuteua namna ya kuwawasilisha wahusika wake. Mbinu rejeshi imekuwa mwafaka kwa mwandishi Habwe kuwabainisha wazimu katika familia hii.

Katika *Kovu Moyoni* msanii ametumia mbinu rejeshi katika visa viwili kama ifuatavyo:

> *"Nilfreda alikumbuka usiku Jumaa alipofika kwao nyumbani na genge la watu kuwafanyia vitendo vya kinyama. Itakuwaje mwenzangu, Jumaa anitendee mimi na hata mama yangu kitendo kile? … Lakini leo analala porini kila siku analia kama mlio wa bunduki au bomu. Halafu analia kilio cha mtu anayeuawa… Nilfreda alishangaa jinsi wakati unavyoweza kulipa matendo ya mtu aliyoyafanya jana…" (uk 109) "Kwa muda walikaa pale mwembeni wakisema, wakicheka. Walipata nafasi ya kurudi katika mateso ya nyuma. Yuko vipi, mambo? Edda aliuliza. Mambo maisha ni kama yamemwendea segemnege. Ameshikwa na wazimu*" (uk 127).

Mbinu rejeshi imetumika kubainisha mhusika wazimu kwa kuangaza kisababishi. Hapa mwandishi ameturejesha nyuma katika tukio la awali ambapo mhusika alitenda kitendo cha kinyama kisha kutuelekeza katika athari ya kitendo hicho kinachoonekana sasa. Jumaa ni wazimu.

Mwandishi amefaulu kutumia mbinu rejeshi kuwabainisha wahusika wazimu. Kwingineko twapata wahusika waliotenda maovu wakitubu na kumwomba Mungu msamaha kama ilivyokuwa kwa mhusika Nandi katika *Cheche za Moto*.

### *Maswali ya Balagha*

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) maswali ya balagha ni mbinu ya kuyatumia maswali ambayo hayahitaji majibu ili kulisisitiza jambo fulani. Nyamari (2016) anasema kuwa jibu la swali la balagha huwa akilini mwa anayeulizwa au anayesoma kazi husika au huwa tayari analijua. Mhimili wa nadharia ya umitindo, ni kuwa lugha inayotumiwa inaweza kuwatambulisha wahusika. Msanii Habwe ametumia mbinu hii kuwabainisha wahusika wazimu katika vitabu teule vilivyoshughulikiwa katika uchunguzi huu.

Katika kitabu cha *Paradiso* msanii ametumia maswali ya balagha katika kisa cha Musa na Joshua. Maswali haya yanatufanya kuelewa kuwa mwendawazimu pia anaweza kukosoa matendo maovu ya watu wenye akili razini na kwamba pamoja na wazimu wake Musa anawatambua Joshua na Lona.

> *"Nyinyi ni nani?... wahubiri gani?"… Maneno ya wazimu hayakumtoka Joshua. Aliendelea kuyatafakari hata baada ya siku ile. "Kwanini ni wazimu lakini alielewa zaidi? Ama ni kweli ulivyosemwa hata Shetani wanaweza kuona ukweli wa mambo?"* (uk 75 na 76)

Mwamanda (2008) anaeleza kuwa tamathali za semi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

ni maneno ambayo hutumiwa na waandishi wa kazi za fasihi ili kutia nguvu katika maana. Matumizi ya maswali ya balagha hapa yamebainisha Musa kuwa wazimu. Joshua na Lona wanashangazwa na maswali hayo lakini wanajua Musa ni wazimu. Nadharia ya umitindo inazingatia dhima ya lugha kumbainisha mhusika (Senkoro, 1987)

Katika *Cheche za Moto* maswali balagha yanaelekeza mkono wa lawama kwa serikali kusababisha kifo cha mwanasiasa na hivyo kuchangia mamake kuwa wazimu. Maswali hayo ya balagha yanaulizwa na mamake Muga:

> *"Tangu mama mwenye kumzaa alpopata habari za mwanawe alikuwa hali, halali. 'Kwanini watu wakuu katika nchi yetu wanakufa hivi?' Alijiuliza. 'Kwanini hakujawa na habari ya serikali kuhusu kupotea kwa huyu Bwana?*" (uk 139).

Katika *Safari ya Lamu* msanii anasema:

> *"Maisha kweli ni kitendawili. Ni vipi mwendawazimu mmoja aliona ni bora kuliko mwenda wazimu mwingine? Ni vipi mwendawazimu atakuwa na utashi kama huo? Ama ni kweli alivyoniambia yule Bwana kifyefye kuwa pia nao ni watu, wala, wanywa…" "Unadhani mimi ni wale hawara zako? Utanipa nini wewe maskini wa Mungu?... Huwezi kununua nguo. Sasa nguo yangu yatoka Dubai utaweza?"* (uk 53).

Matumizi ya maswali ya balagha yamebainisha wazimu. Mwanzo kwa maoni yake kama msimulizi kisha kupitia kwa mhusika wazimu mmoja wao anayeuliza mwenzake maswali kuhusu nguo ilhali wote hawana nguo.

## HITIMISHO

Lengo la Makala hii ilikuwa ni kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumiwa kuwabainisha wahusika wazimu katika riwaya teule za Habwe. Mbinu za Sanaa na tamathali zifuatazo za usemi zimechanganuliwa: Maelezo ya mwandishi, Istiari, Tabaini, Misemo, Ritifaa, Uzungumzi nafsia, Tashbihi, Taswira, Mbinu rejeshi, na Maswali balagha. Utafiti huu umedhihirisha jinsi msanii alivyotumia mbinu hizo kubainisha wahusika wazimu katika riwaya zake.. Utafiti huu ulidhihirisha kwamba tamathali mbalimbali za lugha zinaweza kutumiwa kuwabaini wahusika wazimu.

## Mapendekezo ya Utafiti

Makala hii inapendekeza kuwa wanajamii waepukane na mambo yanayoweza kuchochea wazimu kwao na kwa wengine. Taasisi husika wahakikishe matibabu kwa wagonjwa wa kiakili huku serikali ikiimarisha uchumi na kubuni nafasi za kazi zinazoafikiana na idadi ya vijana wanaofuzu. Aidha Makala hii inapendekeza utafiti wa mbinu za lugha zinazowabaini wahusika wazimu katika kazi za waandishi wengine. Urazini wa wahusika wazimu katika riwaya au tamthilia

## MAREJEEO


Bally (1909) *The origins of translational Equivalents:* Translated and edited by Anthony Pym (2022) Routlege UK.

Bollo (2020) *Utafiti nyanjani: Ukusanyaji wa data ya fasihi simulizi* https://www.youtube.com/channel/UC3EEBQNhW-y6VNg3JgpN76Q

Chiduo, F na wengine (2016) *Kamusi Elezi ya Kiswahili:* The Jomo Kenyatta Foundation; Nairobi

Feder, L. (1980). *Madness in Literature*. Princeton University Press U.

Filson, C. (2014*). Portrayals of Mental Illness in Literature, From Tennyson to Today*. http://talonbooks.com/meta-talon/portrayals-of-mental-illness-in-literature-from-tennyson-to-today

Flores, D. (2014). Social Realism: The Turns of a Term in the Philippines: http://filozofskivestnik online.com/index.php/journal/article/viewFile/1

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

64/150; http://www.journals.uchicago.edu/doi/pdfplus/10.1086/674189

Gelder, M. G., Mayou, R., & Cowen, P. (2001). *Shorter Oxford textbook of psychiatry* (Vol. 4). Oxford: Oxford University Press.

Gromov, M. D. (2018). Three novels of John Habwe: Social criticism through "new enlightenment". *Journal of Language, Technology & Entrepreneurship in Africa*, *9*(1), 90- 101. *https://www.ajol.info/index.php/jolte/article/view/170520*

Habwe, J. (2005) *Paradiso*: Jomo Kenyatta Foundation Nairobi Kenya.

Habwe, J. (2008) *Chche za Moto,* Jomo Kenyatta Foundation Nairobi Kenya.

Habwe, J. (2011) *Fumbo la Maisha*, Jomo Kenyatta Foundation Nairobi Kenya.

Habwe, J. (2011) *Safari ya Lamu*: Sasa Sema (Longhorn), Narobi.

Habwe, J. (2014) *Kovu Moyoni*: Book Mark Africa Publishers Nairobi.

Habwe, J. (2016) *Curr. Vitae:* https://profiles.uonbi.ac.ke/h_john/files/prof._john_habwes_c.v._-_2016.pdf

Kahigi (1994). *Lugha katika vitabu vya watoto. Katika Kahigi K.K (Mh), Kioo cha Lugha*: Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu, Na. 1. (Uk. 21-36)

Kemunto (2016) *Mtindo Katika Utenzi wa Katirifu:* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kombo, D.&Tromp (2006) *Proposal and Thesis Writing - An introduction:* Pauline Pub. Nairobi.

Kramer, L. (2014). Hamlet: The Motif of Madness: https://prezi.com/hfyob9gzhrpm/hamlet-the-motif-of-madness/

Kovacevic, R (2021) Mental Health : Lessons Learnt in 2020 for 2021 and forward: https://blogs.worldbank.org/health/mental-health-lessons-learned-2020-2021-and-forward Retrived on 4th March 2023

Leech, G. N. (1969) *Towards a semantic description of Engish:* Longman Green and co. London

Lemon, L. T., & Reis, M. J. (Eds.). (1965). *Russian formalist criticism: Four essays* (Vol. 405) University of Nebraska Press.

Lugwiri (2011). "*Sitiari, Taashira na Tashbihi katika Utenzi wa Tambuka."* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi ( Haijachapishwa)

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, na Misingi ya Uchambuzi.* Phoenix Nairobi.

Milner, M. (1987). *Suppressed Madness of Sane Men*. Tavistock Publication London.

Morris, S. (2012). Shakespeare's Minds Diseased: Mental Illness and Its Treatment. *The Shakespeare Blog*. http://theshakespeareblog.com/

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam University Press: Dar es Salaam.

Murumba, J. (2013). *Mtindo katika Watu wa Gehenna.* Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi.

Murungi, G. (2013). *Mtindo Unavyoendeleza Maudhui Katika Natala.* Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mwamanda, J. (2008) *Nadharia ya Fasihi Uchambuzi na Uhakiki*, JPD Company & General Supplies Ltd, Da es Salaam.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Nazemi, Z.et al (2022) *New insights into literary topoi*: *A study of 'madness for guilt and remorse;* Razi University (Iran) and University of Córdoba (Spain)

Ntarangwi, M. (2004). Uhakiki wa Kazi za Fasihi. Augustana College: Rock Island

Nyamari, R .K. (2016) *Mtindo Katika Utenzi wa Katirifu:* Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa)

Olson A. (2014) *Illuminating Schizophrenia: Insights into the uncommon mind*. https://www.thriftbooks.com/w/illuminating-schizophrenia-insights-into-the-uncommon-mind_ann-olson/14147337/#edition=60602281

Rono, P. (2013). *Uhakiki wa kimaudhui na kifani Wa kidagaa kimemwozea* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

ROSS, D. W. (1989): «Revising a Map Misread: Hamlet, Romantic Self consciousness, and the Roots of Modern Tragedy». In Dotter, R.L. (ed.): Shakespeare: Text, Subtext, and Context. Selinsgrove: Susquehanna University Press, 107-123.

Senkoro, F. (1982): *Fasihi*. Press and Publicity Centre: Dar es Salaam

Wareing, S., & Thornborrow, J. (1998). *Patterns in language: Stylistics for students of language and literature*. Taylor and Francis.

Veit-Wild, F. (2006). *Writing madness: borderlines of the body in African literature*. James Currey (GB).

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake.* Phoenix Publishers Nairobi

Wamitila, K. (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*: Focus Books, Nairobi

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd, Kenya.

Watuha (2022) *Mwongozo wa Bembea ya Maisha* - Timothy Arege.. Climax Pubishers Nairobi.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.